KUATHIRIWA NA MADINI YA RISASI

HEALTHY HOMES & LEAD POISONING PREVENTION PROGRAM

MADINI YA RISASI KWENYE MAZINGIRA

Madini ya Risasi katika Udongo

Njia Za Kupunguza Madini ya Risasi Katika Udongo

Zingatia maeneo haya ya hatari unapotafuta madini ya risasi katika udongo wako.

Maeneo ya Kuchezea

- Maeneo ya kuchezea yawe mbali na majengo yenye rangi iliyo na risasi
- Panda mimea katika udongo na maeneo ya kuchezea
- Wape watoto sanduku safi la mchanga

Mashamba ya Mboga

- Badilisha inchi za juu ya udongo na udongo safi
- Tia kiasi kidogo cha maji udongoni ili upunguze vumbi
- Osha mboga zozote zilizopandwa shambani kabla ya kuzikula
- Hakikisha udongo hauna asidi nyingi
- Vaa glavu unapofanya kazi udongoni

Sehemu inayodondokewa na rangi

- Sehemu inayodondokewa na rangi ni eneo la futi 3 linalozingira nyumba
- Eneo hili huwa na viwango vya juu zaidi vya risasi kutokana na rangi ya nje kubambuka na kuanguka
- Ondoa inchi 10 za juu za udongo hapo
- Panda mimea inayozunguka nyumba ili watoto wasiende hapo
- Weka ua katika eneo au funika kwa matandazo ya mandhari

Njia za wanaotembea kwa miguu

- Usilete uchafu wenye madini ya risasi kutoka njiani hadi nyumbani

MADINI YA RISASI KATIKA UDONGO NI TATIZO

Njia pekee ya kujua ikiwa kuna madini ya risasi katika udongo ni kuupima

Watu wengi wakisikia kuathiriwa na madini ya risasi, huwa wanafikiria rangi ya zamani, lakini risasi udongoni inaweza pia kuwadhuru watoto. Risasi iliyoko udongoni hutoka kwenye rangi inayobanduka, uchafu wa kiwanda kuwepo kwa miaka na petroli yenye risasi magarini. Lead arsenate pia ilitumiwa kama kiuadudu mashambani. Risasi ikiingia udongoni, haihamishwi wala haiyeyuki; inadumu milele.

HATARI KWAKO NA KWA FAMILIA YAKO

Unaweza kufikiwa na risasi udongoni kwa njia nyingi

- Mara nyingi watoto hucheza udongoni na matopeni, na wanaweza kuweka uchafu wenye madini ya risasi midomoni, mikononi na usoni
- Watu huleta madini ya risasi kutoka nje katika viatu vyao
- Wanyama wanaweza kuleta uchafu wenye madini ya risasi nyumbani katika manyoya na miguu

KUILINDA FAMILIA YAKO

Madini ya risasi udongoni ni hatari na inaweza kuingia nyumbani

- Panda mimea, vichaka, na mimea ya kufunikia ardhi itakayowazuia watoto kuwa katika udongo usio na mimea
- Weka zulia katika kila mlango ya kuingia ili uzuie udongo kuingia
- Vua viatu mlangoni
- Nawa mikono na kucha baada ya kucheza nje
- Osha vya vifaa vya kuchezea watoto uwanjani

Idara ya NH ya Afya na Huduma kwa Wanadamu, Kitengo cha Huduma za Afya ya Umma

1-800-897-LEAD

Kuathiriwa na Madini ya Risasi

HEALTHY HOMES & LEAD POISONING PREVENTION PROGRAM

Madini ya Risasi kwenye Mazingira

Madini ya Risasi kwenye Maji

Punguza Hatari

Ni vigumu sana kupata madini ya risasi kwenye maji ya kunywa ya umma, na kuna uwezekano mkubwa kwamba inaingia kwenye maji yako kupitia mabomba na ufundi bomba wa nyumbani mwako.

- Tumia tu maji baridi kupikia na kunywa
- Usidhubutu kutumia maji ya moto kutoka mferejini kutayarishia chakula cha mtoto
- Kuchemsha maji HAKUONDOI madini ya risasi. Kuchemsha maji huenda kukasababisha risasi kukolea zaidi
- Tumia maji yaliyochujwa ama ya chupa ikiwezekana
- Ikiwa unatumia chujio la maji, hakikisha limethibitishwa kwamba linaondoa madini ya risasi na ubadilishe machujio mara kwa mara
- Badilisha sehemu za ufundi bomba za nyumbani zenye madini ya risasi
- Hakikisha kwamba ukarabati wa mabomba hautumii mseto wa vyuma ya risasi
- Zoea kutiririsha maji katika kila mfereji kabla ya kuyatumia, hasa asubuhi
- Epusha watoto kunywa maji kutoka kwa mipira ya maji, kwa vile ngozi ya plastiki iliyoko kwenye mipira ya

VYANZO VYA RISASI MAJINI

Madini ya risasi yanaweza kuingia majini kupitia mabomba

Mabomba ya madini ya risasi yalitumiwa sana mpaka miaka ya 1940. Mseto wa risasi wa kuunganisha vyuma ulitumiwa mabombani mpaka 1986. Bado inapatikana mabombani mwa nyumba nyingi za zamani. Katika nyumba ya zamani yenye mabomba ya madini ya risasi na mseto wa vyuma, risasi hii inaweza kuingia kwenye maji yako na wewe na familia yako mnaweza kuikunywa.



Madini ya risasi yanaweza kuingia majini kupitia vyanzo vya nyumbani kama:

- Kuchakaa kwa mabomba, mifereji, zana na mseto wa vyuma
- Shaba na mifereji iliyopakwa kromiamu
- Hodhi ya zamani yenye miguu kama ya mnyama

UPIMAJI

Huwezi kuona, kunusa ama kuonja madini ya risasi kwenye maji

Njia pekee ya kujua ikiwa maji yako yana madini ya risasi ni kuyapima. Ikiwa unataka kupima madini ya risasi kwenye maji yaliyoko nyumbani mwako, wasiliana na Maabara ya Idara ya Huduma za Mazingira ya NH namba ni (603)-271-3445. Ukipata madini ya risasi, hakikisha kwamba umeondoa haraka vyanzo hivyo vinavyochafua maji kwa risasi .

UNACHOWEZA KUFANYA

Bubujisha maji kwenye mabomba yako

- Maji yasipotumiwa kwa saa 6-8, madini ya risasi kutoka kwenye mabomba na tangi la maji inaweza kupenyezea majini
- Hakikisha umewacha maji baridi yatiririke kwa angalau sekunde 30 hadi dakika 1 kabla ya kutumia maji yaliyosalia kwa muda mrefu
- Kwa maji ya moto, acha maji yatiririke kwa sekunde